THE AFRICA WE WANT (AFRIKA TUNAYOITAKA)

Afrika tunayoitaka ni Afrika ya amani, utawala bora, haki, usawa wa jinsia,na maendeleo katika uchumi na viwanda .Tufike mahali Afrika iwe tena sio bara la giza kama ilivyozoeleka karne zilizopita, bali pawe mahali ambapo mataifa na mabara yote yatakimbilia kutafuta ajira, mitaji, teknolojia, ushauri hata ujuzi kutoka kwetu. Tufike mahali ambapo mataifa yote watapendelea kununua bidhaa na kutumia huduma kutoka Afrika. Tufikirie juu ya uvumbuzi na ubunifu mbalimbali utakaoweza kuufanya uchumi wetu kukua zaidi ya ule wa mataifa yaliyoendelea. Tufikirie kuvumbua ndege zenye kutumia nishati ya jua pekee inayoweza kujichaji maradufu na kutumika nyakati za usiku ikiwa na ufanisi mkubwa kama ule wa wakati wa jua (mchana). Hii yote ni kufikiria njia mbadala ya kuwa wabunifu huku tukiwapiku wazalishaji wapinzani ambao ndege zao zitakua na gharama kubwa ya kuziendesha tofauti na zetu kwa kuwa zao zinatumia mafuta. Wakuanzisha na kufanya haya yote ni mimi na wewe. Insha yangu inawalenga zaidi vijana ambao ndio nguvu kazi ya taifa na chachu ya maendeleo, pia maendeleo haya yote ni kwa ajili ya manufaa yao na vizazi vyao vijavyo.

Ajenda 2063 iliyotungwa na Umoja wa Afrika (AU), ina malengo ya kuhakikisha utekelezaji wa jitihada za kuhakikisha kuwa maendeleo endelevu Afrika yanatimizwa ipasavyo. Ajenda hii inajadili gurudumu la maendeleo kuendeshwa na watu (mimi na wewe) badala ya kutegemea jitihada za serikali pekee. Afrika tunayoitaka ya kuwa na gurudumu la maendeleo kuendeshwa na watu itapatikana endapo mambo haya ya msingi yatatekelezwa na kila mmoja wetu na sio serikali pekee;

Kuanza kuzalisha kwa kile ulichonacho. Uzalishaji ndio muhimili wa uchumi wowote hapa Afrika, na ndio chanzo cha viwanda. Hata mataifa yaliyoendelea, yamefika hapo kwa kuwa watu wake wanazalisha ipasavyo. Kama kila kijana atazalisha, uchumi wa nchi za Afrika lazima upande. Uzalishaji kwa mtu mmojamoja sio lazima uanze na mtaji mkubwa. Chochote ulichonacho, hata kama ni Tsh 2000, zinatosha kabisa kuanzisha biashara,kulima au hata kufuga. Vijana wasio na ajira wala mitaji wanaweza kuanzisha biashara ndogondogo hata ile ya kuuza pipi na karanga barabarani ilimradi izae faida. Biashara hizi lazima zikue kadri siku zinavyoenda na mtaji wake nao pia utapanda. Hata wale wenye ajira, lazima wasiegemee upande mmoja wa ajira pekee. Lazima wajihusishe na ujasiriamali wa aina yoyote kulinga na vipaji, ujuzu au uwezo waliokua nao juu ya kumudu biashara fulani. Kama kila mmoja kwenye jamii atazalisha, basi tatizo la ukosefu wa ajira lilokithiri kwenye nchi nyingi za Afrika ikiwemo Tanzania lazima liishe. Pia vitendo vya ujambazi na uny'ang'anyi kwenye jamii

lazima navyo vipungue. Jamii za Afrika zitaishi kwa amani na maendeleo yataonekana kwa kuwa pato la taifa litaongezeka. Ili kutimiza haya ni wajibu wa kila mwananchi kujifunza elimu ya ujasiriamali ili kujikimu na maisha. Katika jamii ijulikane kuwa kijana asiyezalisha (kufanya kazi) hana manufaa yoyote ya kuleta maendeleo ya jamii, taifa na Afrika kwa ujumla. Ushauri kwa serikali ni kuliangalia jambo hili kwa jicho la pili nikimaanisha, kutunga sera ambazo zitawajibisha vijana wote wasiopenda kujishughulisha. Sera hizi zaweza kuwa ulipaji wa kodi kubwa, faini au penati kama adhabu.

Afrika tunayoitaka ni ile yenye utawala bora. Afrika yenye utawala bora ndio chachu ya maendeleo endelevu. Utawala bora ni ule unaozingatia haki, usawa, demokrasia, utamaduni na maadili ya jamii. Afrika tunayoitaka ni ile isiyokuwa na chokochoko za kisiasa, vita, ubaguzi wa rangi, dini wala kabila. Viongozi wa Afrika wasichoke kuelimisha jamii juu ya utawala wa amani usio na vita, ubaguzi, au chokochoko za kisiasa. Ni jukumu letu sote kuhakikisha kuwa tunakuwa mabalozi wa amani, demokrasia, usawa, na tunasimamia maadili na utamaduni wa jamii zetu za kiafrika. Uajibikaji na uaminifu wa viongozi ndio silaha ya utawala bora uliobeba maendeleo ya Afrika.

Afrika tunaayoitaka ni Afrika iliyo huru dhidi ya ujinga, maradhi na umaskini. Baba wa taifa la Tanzania, Mwalimu Julius K Nyerere aliainisha maadui wakubwa watatu wa maendeleo ambao ni ujinga, maradhi na umaskini. Mataifa mengi ya Afrika ikiwemo Tanzania, yanashindwa kuendelea kufikia uchumi wa kati kwa sababu ya ujinga, maradhi na umaskini uliokithiri. Umaskini ndio adui mkubwa anayeangamiza maendeleo ya jamii. Afrika tunayoitaka ni Afrika iliyohuru kabisa, iliyo mbali na ujinga, maradhi na umaskini kwa watu wake. Hivyo, ni wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa maadaui hawa tunawaangamiza katika jamii zetu ili tupate maendeleo endelevu ya taifa na Afrika kwa ujumla.

Mimi kama kijana wa Tanzania, nina wajibu wa kujenga Afrika tunayoitaka kwa kuwa mabadiliko yanaanza na mimi. Juhudi zangu zitashawishi na wengine kuwa na muamko wa kuijenga Afrika kuwa bara la nuru na sio giza tena. Kwa kutambua hili nimefikiria kuanzisha taasisi inayoitwa VIJANA NA MAENDELEO AFRIKA (VIMA). Taasisi hii itafanya kazi kuu ya kuhamasisha vijana katika utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu (SDGs) yaliyoanzishwa na Umoja wa mataifa (UN). Taasisi hii isiyo ya kifedha, itakuwa na blogi ambayo vijana watapata ushauri, elimu ya kujitambua pamoja na fursa mbalimbali. Kutakua na kurasa kwenye mitandao ya kijamii kama FACEBOOK, TWITTER na INSTAGRAM ili kuwafikia vijana wote Afrika. Katika kuhamasisha utekelezaji wa malengo ya maendeleo

endelevu, VIJANA NA MAENDELEO AFRIKA itafanya yafuatayo ili kujenga Afrika tunayoitaka 2063;

1) Kutoa elimu ya kujitambua kwa vijana. Hii itahusisha elimu ya uzazi na kuacha ngono zembe. Mimba za utotoni, magonjwa ya kuambukiza kama UKIMWI na Kaswende yanachangia kwa kiasi kikubwa kudhorota kwa maendeleo Afrika. Vijana wanahitiji elimu ya kujitambua ili kuepusha mimba zisizotarajiwa pamoja na magonjwa yanayoua vijana kwa wingi.
2) Kutoa elimu ya ujasiriamali na kufundisha ujuzi mbalimbali. Taasisi hii itafundisha vijana wa Afrika juu ya umuhimu wa kufanya ujasiriamali. Itawafundisha pia ujuzi mbalimbali wa biashara, kazi na ufundi, kupitia semina, mikutano au video zitakazokuwa zinatumwa mtandaoni. Vijana watafundishwa jinsi gani wanaweza kuongeza vipato vyao kupitia simu zao za mikononi balada ya kutumia muda mwingi kwenye kurasa za udaku.
3) Kusaidia vijana kupata masoko ya bidhaa zao wanazozalisha. Tutawasaidia kutangaza bidhaa na huduma za vijana wanaozalisha kwa weledi na ubora.
4) Kuendesha mashindano ya ubunifu na uvumbuzi ili kuwasaidia vijana kuwa wabunifu kwenye nyanja mbalimbali. Kupitia hili tutaweza kufanikisha hata lile wazo la kutengeneza ndege yenye kutumia nishati ya jua pekee.
5) Kusaidia vijana wenye vipaji kukuza vipaji vyao. Kazi zao zitaonekana kila mahali kupitia blogi na kurasa zetu za mitandao ya kijamii.
6) Kukumbusha vijana juu ya umuhimu wa kutunza na kuthamini utamaduni wetu na kuacha kugeza tamaduni na ustarabu wa mataifa ya nje ya Afrika.

Afrika tunayoitaka itapatikana endapo mambo yaliyotajwa yatafanyiwa kazi. Ni jukumu langu na lako pia, kuhakikisha Afrika inakuwa ni mahali salama penye maendeleo. Natoa rai kwa taasisi, serikali, Umoja wa Afrika na watu wenye mapenzi mema na Afrika, kusaidia katika kufanikisha VIJANA NA MAENDELEO AFRIKA (VIMA) kuanzishwa ili tupate Afrika tunayoitaka yenye maendeleo endelevu ifikapo mwaka 2063. Kupitia VIMA, juhudi za kuleta maendeleo ya Afrika kupitia kijana mmojammoja wa kiafrika, itakuwa ni zaidi ya nguvu atumiazo simba kuwinda nyikani ili ashibe. Wito (motto) wa VIMA ni, " Maendeleo ya Afrika, jukumu la kijana, vijana tuchukue hatua".

Imeandikwa na GRACE MARTIN NAKOMOLWA, kutoka Dar es Salaam Tanzania.